Namba ya Mtahiniwa.....

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI

015 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

Muda: Saa 2:30 **Jumatatu, 18 Novemba 2019 mchana**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **saba (7)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Majibu yaandikwe kwenye nafasi ulizopewa.
4. Andika kwa kutumia kalamu yenye wino wa bluu au mweusi.
5. Vifaa vyote vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU		
NAMBA YA SWALI	**ALAMA**	**SAINI YA MTAHINI**
1		
2		
3		
4		
5		
6		
7		
JUMLA		
SAINI YA MHAKIKI		

1 819015 000016

Scanned by CamScanner

Namba ya Mtahiniwa.....

BISMILAHIR RAHMANIR RAHIM

SEHEMU A (Alama 20)

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kisanduku.

(i) Mapokezi au taarifa ya yale yote aliyoyafanya Mtume (s.a.w) au yaliyotendwa mbele yake na akayaridhia hujulikana kama

A Hadithi. B Hadithi ya Mtume.
C Sunnah. D Sunnah ya Mtume.

(ii) Msingi ambao ulitumika kama rejea katika kumfahamu msimulizi wa Hadithi mkweli na asiyekuwa mkweli ni

A Aljarh. B Aljarhi wataadil.
C Ataadil. D Isnadi.

(iii) Sehemu ya masimulizi ya Hadithi tokea kwa Mtume (s.a.w) au swahaba hadi kuandikwa kwake hujulikana kama

A Rawi. B Matini.
C Riwaya. D Isnadi.

(iv) Uandishi wa Hadithi katika kipindi cha wafuasi wa Maswahaba ulianza kipindi gani?

A 11 A.H - 101 A.H. B 11 A.H - 100 A.H.
C 101 A.H - 200 A.H. D 101 A.H - 201 A.H.

(v) Mtume (s.a.w) amesema "Hakika kuswihi kwa amali kutategemea nia". Katika Hadithi hii tunajifunza nini?

A Nia hujulikana kutokana na matendo anayoyafanya mtu.
B Nia katika ibada ni lazima itamkwe kwa sauti.
C Nia si lazima iambatane na matendo.
D Amali njema hulipwa kutokana na nia aliyoitanguliza.

(vi) Nini maana ya Hadithi Qudusiyy?

A Ni Hadithi ya uongo aliyozuliwa Mtume (s.a.w).
B Ni habari au usemi alioutoa Mtume (s.a.w) kama alivyoupokea kutoka kwa Allah (s.w) lakini ulio nje ya Qur'an.
C Ni usemi au habari aliyoitoa Mtume (s.a.w) mwenyewe.
D Hadithi ambayo wapokezi wake wote ni watu waadilifu.

Scanned by CamScanner

Namba ya Mtahiniwa.....

(vii) Kiongozi aliyeongoza mwaka 99-101 A.H na kuchukua dhima ya kuchuja na kuandika Hadithi zilizo sahihi ni

A Omar bin Abdul Aziz. B Omar bin Khatab.
C Ummaya bin Sufian. D Hamza bin Abdu – Muttalib.

(viii) Miongoni mwa njia waliyotumia wanazuoni wa Hadithi kuzitambua Hadithi za uzushi ni

A wapokezi wake kutokuwa katika muhajirina.
B wapokezi wake kuchelewa kuingia katika Uislamu.
C Hadithi kutokuwa mashuhuri.
D Hadithi kwenda kinyume na Qur'an.

(ix) Historia ya kuhifadhiwa Hadithi katika maandishi imegawanyika katika hatua ngapi?

A Mbili B Tatu
C Nne D Tano

(x) Kitabu cha Hadithi cha Sunan Ibn Majah kiliandikwa na nani?

A Imamu - al – Bukhari B Imamu Muslim
C Abu Daud D Muhammad bin Yazid

Scanned by CamScanner

2. Oanisha maneno kutoka **Orodha B** na sentensi kutoka **Orodha A** kisha jaza herufi yake katika jedwali.

Orodha A		Orodha B
(i)	Viumbe wa Mwenyezi Mungu walioumbwa kutokana na nuru.	A Majini
(ii)	Kitabu kilichoteremshwa kwa Nabii Musa (a.s).	B Qadar
(iii)	Malaika anayehusika na utaratibu wa kunyesha mvua hapa duniani.	C Jibril (a.s)
		D Iman
(iv)	Kitabu kilichoteremshwa kwa Nabii Daud (a.s).	E Injil
(v)	Nguzo ya sita ya Imani ya Kiislamu.	F Israil
(vi)	Malaika atakayepuliza baragumu siku ya kufishwa na kufufuliwa kwa viumbe wote kwa idhini ya Allah (s.w).	G Qur'an
		H Zabur
(vii)	Malaika mwenye kupeleka ujumbe kwa mitume.	I Israfil
(viii)	Malaika aliyepewa dhamana ya kutoa roho za viumbe.	J Taurat
(ix)	Viumbe walioumbwa kwa ajili ya kumuabudu Allah (s.w) kama ilivyo kwa binadamu.	K Tawhiid
		L Ibilisi
(x)	Kuwa na yakini moyoni juu ya kuwepo kwa jambo usiloliona lakini kuna dalili za kutosha juu ya kuwepo kwake.	M Allah (s.w)
		N Malaika
		O Mikail

Majibu

Orodha A	(i)	(ii)	(iii)	(iv)	(v)	(vi)	(vii)	(viii)	(ix)	(x)
Orodha B										

SEHEMU B (Alama 40)

3. Andika **KWELI** kama sentensi ni sahihi au **SI KWELI** ikiwa sentensi si sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Wasioamini kuwepo kwa Allah (s.w) hawana dini.....

(ii) Katika Uislamu hakuna mgawanyo wa elimu ya dini na dunia.....

(iii) Malaika ni viumbe wasio na matamanio ya kijinsia.....

(iv) Kuamini siku ya mwisho ni katika nguzo za Uislamu.....

Scanned by CamScanner

(v) Kila aliyetamka shahada mbili ni muumini.....

(vi) Makafiri wanaamini kuwa dini ni chombo cha kumkandamiza mwanadamu.....

(vii) Tawhiid ni elimu inayofundisha kumuabudu Allah kama inavyotakiwa.....

(viii) Chanzo cha dini zote ni Mwenyezi Mungu mwenyewe.....

(ix) Uislamu unahimiza kusoma fani za elimu zote.....

(x) Makafiri ni watu wasio na dini.....

4. Kwa kutumia maneno uliyopewa, chagua jibu sahihi ili kujaza nafasi wazi katika vipengele (a) – (j).

Ali bin Abutwalib, mwenye kushukuriwa, khazraj, Taif, Isra, Miraj, Yathrib, Mtume (s.a.w), Abu Jahal, Khadija, Halima bint Abi-Dhuaby, Aqaba, masanamu, Amina bint Wahhab, mwenye nguvu.

(a) Kiongozi wa mkutano mkubwa katika "Dar-al-Nadwa" wa kumdhuru Mtume (s.a.w) kabla ya kuhamia Madina aliitwa.....

(b) Mji wa Madina kabla ya hijra ya Mtume (s.a.w) ulijulikana kama.....

(c) Swahaba aliyekabidhiwa amana zote za watu alizokuwa nazo Mtume (s.a.w) ili azirudishe kwa wenyewe wakati Mtume (s.a.w) anahama kuelekea Madina ni.....

(d) Mahali palipofikiwa makubaliano baina ya Mtume (s.a.w) na watu wa Yathrib palijulikana kama .....

(e) Safari ya Mtume (s.a.w) kutoka msikiti mtukufu wa Makkah mpaka msikiti wa Jerusalem (Baitul muqadas) ilijulikana kama .....

(f) Kitu ambacho Mtume (s.a.w) alichukia sana tangu utotoni mwake ni.....

(g) Jina la Muhammad alilopewa Mtume (s.a.w) na babu yake maana yake ni.....

(h) Mlezi wa Mtume (s.a.w) aliyetokea katika kabila la Bani Khawaizin ambalo lina sifa ya usafi na ufasaha wa lugha ya kiarabu alikuwa anaitwa.....

(i) Kiongozi mwenye tabia njema isiyo na mfano wake katika jamii yake ni.....

Scanned by CamScanner

(j) Mwanamke mjane miongoni mwa matajiri wakubwa wa Makkah aliitwa.....

5. Nukuu zifuatazo **hazikupangwa** katika mtiririko unaotakiwa. Panga nukuu hizo katika mpangilio sahihi ili kupata maana iliyokamilika.

(a) Historia ya kushuka Qur'an kwa Mtume Muhammad (s.a.w) kupitia kwa malaika Jibril (a.s) inasimuliwa vyema na Bibi 'aisha (r.a) katika Hadithi ifuatayo:
(i) Basi alikuwa anakwenda jabar Hira akifanya ibada masiku mengi na alichukua masurufu kwa ajili hiyo.
(ii) Kilichoanza katika wahyi wa Mtume (s.a.w) ni ndoto za kweli.
(iii) Masurufu haya yalipokwisha alirudi tena kwa Bibi Khadija aliyemtayarishia masurufu kama yale (ya kwanza) mpaka ikambainikia haki akiwa pangoni Hira.
(iv) Kisha akaona ni bora kujitenga.
(v) Alikuwa Mtume (s.a.w) haoti chochote isipokuwa kilitokea kama alivyoota.

Majibu

1	2	3	4	5

(b) Dalili kwamba binadamu tunahitaji ulinzi wa Mwenyezi Mungu (s.w) dhidi ya shari mbalimbali.
(i) Nashari ya alivyoviumba.
(ii) Nashari ya hasidi anapohusudu.
(iii) Sema: ninajikinga kwa Mola wa ulimwengu wote.
(iv) Nashari la giza la usiku liingiapo.
(v) Nashari ya wale wanaopulizia (vivia) mafundoni, (wakavunja mashikamano yaliyo baina ya watu, yaani shari ya mafatani)

Majibu

1	2	3	4	5

Scanned by CamScanner

SEHEMU C (Alama 40)

6. Jibu maswali yote kwa ufupi.

(a) (i) Nini maana ya ibada?

.....

.....

.....

.....

.....

(ii) Taja mambo mawili katika ibada ambayo Muislamu akiyafanya binadamu wengine watafaidika.

- .....

  .....

- .....

  .....

(b) Toa tofauti mbili baina ya utekelezaji wa Swala za faradhi wakati wa kawaida na ule wakati wa vita.

(i) .....

.....

.....

(ii) .....

.....

.....

(c) Taja sharti nne za Swala ambazo Muislamu anapaswa kuzichunga kabla hajaanza kuswali.

(i) .....

(ii) .....

(iii) .....

(iv) .....

Scanned by CamScanner

(d) (i) Taja aina nne za mali ambazo Muislamu akimiliki analazimika kuzitolea Zakat.

- .....
- .....
- .....
- .....

(ii) Taja aina mbili za Sunnah zinazoambatana na funga ya Ramadhani.

- .....
  .....
- .....
  .....

(e) (i) Eleza maana ya Ihram.

.....
.....
.....
.....
.....
.....

(ii) Ainisha mambo mawili miongoni mwa yaliyoharamishwa kwa mwenye kuwa katika Ihram.

- .....
  .....
- .....
  .....

7. Bainisha makundi ya Waislamu ambao wameruhusiwa kuahirisha kufunga mwezi wa Ramadhani kutokana na dharura zao.

.....
.....
.....
.....

Scanned by CamScanner